*Kioo cha Lugha, Juz. 23(2), 181-205*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i2.2

# Kategoria za Utumwa katika Fasihi ya Kiswahili: Uchunguzi wa Kazi Teule

*Ernesta S. Mosha*[1] *na Grace H. Minja*[2]

## Ikisiri

Utumwa ni mfumo ambao hulazimisha watu kufanya kazi au jambo fulani bila malipo au ridhaa. Kuna aina kuu mbili za utumwa, yaani utumwa wa kijadi na utumwa wa kisasa[3]. Utumwa wa kijadi unahusu watu kuuzwa kama bidhaa na kwenda kutumikishwa sehemu kama vile kwenye mashamba makubwa, migodini na majumbani. Ni utumwa ulioanza zamani sana na ulikuwapo katika jamii kwa karne nyingi. Madhara ya utumwa wa kijadi bado hayajafutika katika historia za jamii husika. Kwa upande mwingine, utumwa wa kisasa ni ule unaojitokeza kwa namna nyingi kama vile: utumwa wa kifikra, kimapenzi, madeni, na kutumikisha watoto wadogo. Aina hii ya utumwa, licha ya kuonekana kuwa umeshika kasi sana katika zama hizi za utandawazi, kwa hakika, baadhi ya aina zake zimekuwa katika jamii kwa muda mrefu. Makala hii imejadili namna fasihi ya Kiswahili inavyosawiri utumwa wa kijadi na aina anuwai za utumwa wa kisasa. Kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini, riwaya nne za fasihi ya Kiswahili - *Uhuru wa Watumwa* (1934), *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1987), *Kwaheri Iselamagazi* (1992) na *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1995) zimechunguzwa ili kuweka bayana suala hili. Imebainika kuwa utumwa wa kisasa una madhara ambayo hayajulikani mapema ikilinganishwa na utumwa wa kijadi kwa sababu madhara hayo hayaonekani waziwazi kwa kuwa yapo ndani ya utu wa mhusika. Pia, utumwa wa kisasa, kama vile utumwa wa kifikra na utumwa wa madeni unachangia katika utokeaji na/au uimarishaji wa utumwa wa kijadi.

## 1.0 Utangulizi

Utumwa, kama mfumo ambao hulazimisha watu kufanya kazi au jambo fulani bila malipo au ridhaa, umekuwapo katika jamii nyingi duniani kwa miaka mingi. Baks,

[1] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
Baruapepe: ernesta.mosha@udsm.ac.tz

[2] Mhadhiri, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: grace.minja@udsm.ac.tz

[3] Aina hizi za utumwa hujulikana pia kama utumwa mkongwe na utumwa mamboleo mtawalia.

Breman na Nooij (1966) wanabainisha sifa za jumla za utumwa kuwa ni nafasi ya chini, utegemezi na kudhalilishwa. Wanaendelea kusema kuwa hali hizi zinawafanya watu walio katika hali ya utumwa (watumwa) kufanya kazi ngumu na zisizoheshimika, za hadhi ya chini na hawana uwezo wa kuvunja uhusiano huo. Pia, watumwa wanakuwa katika hali ya kizuizi cha kudumu kwani huitwa kufanya kazi wakati wowote. Kwa ujumla, sifa hizi zinaonekana kujikita zaidi katika utumwa wa kijadi, pengine ni kutokana na maana ya utumwa iliyokuwapo wakati huo. Utumwa wa kisasa wenyewe unajumuisha aina mbalimbali za vitendo vya unyonyaji vinavyowanyima watu uhuru na haki zao, mathalani, kazi za kulazimishwa, usafirishaji haramu wa binadamu, ajira kwa watoto, utumwa wa madeni na aina nyingine za unyonyaji. Quirk (2012) anaeleza kuwa ili kuweza kubaini hasa kinachosemekana kuwa utumwa katika dunia ya leo, tunahitaji kuzingatia sura mbalimbali ambazo utumwa umekuwa nazo kihistoria.

Makala hii inajadili namna fasihi ya Kiswahili inavyosawiri utumwa wa kijadi na aina anuwai za utumwa wa kisasa. Makala hii imetumia Nadharia ya Mwingilianomatini na riwaya nne za fasihi ya Kiswahili - *Uhuru wa Watumwa* (1934), *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1987), *Kwaheri Iselamagazi* (1992) na *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1995) kudadavua masuala haya.

### 1.1 Umuhimu wa Kuchunguza Kategoria za Utumwa katika Fasihi

Kwa kiasi kikubwa kazi za fasihi zinatokana na yale yaliyomo katika jamii na jamii ni malighafi ya kazi za fasihi (Madumulla, 2000; Mulokozi, 2017). Ingawa baadhi ya kazi za fasihi zinakwenda mbali zaidi ya yale yanayoendelea katika jamii kutokana na ubunifu wa mwandishi, bado tunaweza kujifunza mambo mengi kuhusu maisha ya binadamu kama yanavyosawiriwa katika kazi za fasihi simulizi na andishi. Kwa kuwa utumwa ni hali ambayo ilikuwapo na ipo katika jamii, ni wazi kuwa masimulizi ya watumwa yanaakisiwa pia katika kazi za fasihi. Aidha, fasihi ni chombo muhimu katika kubadilisha historia ya binadamu kwa kueleza uzoefu wa watu walioishi au kusoma simulizi za kitumwa (Moniz, 2014). Hivyo, ni muhimu kuchunguza ni kwa namna gani fasihi ya Kiswahili imejihusisha na masuala yahusuyo simulizi za utumwa. Mathalani, masimulizi ya watumwa ni miongoni mwa kazi za fasihi zinazoeleza uzoefu wa watu waliokuwa watumwa katika kipindi cha utumwa. Baadhi ya simulizi za watumwa ni kama vile *The Interesting Narrative of the Life of Olaudah Equiano* (1789), *The History of Mary Prince, A West Indian Slave, Related by Herself* (1831), *Narrative of the Life of Frederick Douglass, An American Slave, Written by Himself* (1845), *Twelve Years A Slave, Narrative of Solomon Northup* (1853), na *Uhuru wa Watumwa* (1934). Aidha, watunzi wa kazi za fasihi wamechota mbinu za kifani na kimaudhui kutoka katika simulizi za watumwa na vyanzo vingine vinavyozungumzia utumwa na biashara ya watumwa kutoka katika jamii. Katika fasihi ya Kiswahili, kwa mfano, kazi kama *Tendehogo* (1984), *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1987), *Kwaheri Iselamagazi* (1992), *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1995) na nyinginezo zinazungumzia siyo tu utumwa wa kijadi na

biashara ya watumwa Afrika Mashariki, bali pia aina mbalimbali za utumwa kama zilivyobainishwa na watafiti tangulizi. Kwa hiyo, makala hii imechunguza kazi ambazo kinadharia zinafahamika kuwa zinazungumzia utumwa wa kijadi kwa kiwango kikubwa lakini pia zinahusisha utumwa wa kisasa. Lengo la kufanya hivyo ni kuweza kuonesha kuwa, pamoja na kwamba kinadharia zinafahamika kuwa kazi hizi zinahusu utumwa wa kijadi, lakini ni kazi ambazo zimebainika kuzungumzia pia utumwa wa kisasa katika viwango tofauti. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini, makala hii imefafanua kategoria mbalimbali za utumwa zinavyoingiliana na kukamilishana.

## 2.0 Nadharia ya Mwingilianomatini

Mwingilianomatini ni nadharia inayochunguza mwingiliano, mahusiano na utangamano wa kazi au matini za kifasihi katika viwango mbalimbali kama vile fani na maudhui. Ni nadharia inayosisitiza kuwa matini ya kifasihi haiwezi kuwapo katika upweke wake bila kuhusishwa na matini nyingine, na hii inatokana na ukweli kwamba mwandishi wa matini husika huwa msomaji wa matini nyingine kabla hajaandika matini yake. Hivyo, kazi ya sanaa haiwezi kukwepa mwingiliano katika marejeleo, nukuu au kuingiliana kwa maudhui ya aina mbalimbali (Alfaro, 1996; Worton na Still, 1990). Dhana kuu katika nadharia hii ni kuwa hakuna matini ya kifasihi inayoweza kujitegemea bila kuhusiana na matini nyingine. Kwa hiyo, msanii hutunga matini yake kutokana na matini za awali. Hii ina maana kuwa mwandishi hubuni matini maalumu au ya kiutamaduni kutokana na malighafi ambayo haiwezi kutenganishwa. Jambo hili linaibua uhusiano baina ya mtunzi, kazi, msomaji, jamii na historia (Kristeva, 1969). Aidha, matini yoyote ile haitumii matini za awali kama zilivyo bali huzibadilisha, hali ambayo inaleta ugumu kutambua asili yake. Hii ina maana kuwa matini hujengwa upya, hutilia mkazo yale yanayolengwa katika matini husika huku ikiwa mwangwi wa matini za awali. Hali hii hujenga historia na kuchangia mabadiliko mengi katika matini, huku zikitazamia kujenga matini za baadaye (Bakhtin, 2010). Kwa mfano, Bakhtin alishikilia mtazamo kwamba maandishi ya kifasihi hayawezi kutenganishwa na maandishi ya kijamii na kitamaduni ambayo ni mandhari inayotumiwa na mwandishi kuunda matini fulani.

Wamitila (2008) anabainisha mwingiliano unaoweza kujitokeza katika kazi za fasihi kama vile mwingiliano wa kiurejelezi ambapo matini au kazi za kifasihi huhusiana na kazi nyingine zilizoitangulia. Hii ina maana kuwa mwingiliano huo unaweza kuwa katika fani au maudhui na unaweza kuwa chanya au hasi kulingana na malengo ya mwandishi. Wamitila anasisitiza kuwa katika Nadharia ya Mwingilianomatini ni muhimu kuchunguza mahusiano yenyewe na kuonesha ni kwa namna gani ambavyo mahusiano hayo yanaathiri sifa tofauti za kazi inayorejelewa. Mulokozi (2017) anaongeza kuwa Kristeva aliipanua dhana ya Bakhtin (dayalojia au usemezano) na kusisitiza kuwa, kwa mujibu wa Nadharia ya Mwingilianomatini, kazi ya fasihi huweza kuwa na sauti zaidi ya moja. Hii ina maana kuwa fasihi yoyote husemezana na fasihi iliyokuwapo kabla yake na fasihi

itakayokuja baada yake. Hivyo, kila kazi ya fasihi huingiliana na kuathiriana na kazi nyingine tangulizi. Kwa kutumia mawazo ya Nadharia ya Mwingilianomatini, makala hii imebaini mwingilianomatini uliojitokeza katika vipengele mbalimbali vya kimaudhui vya matini zilizochambuliwa. Mathalani, tumeona namna utumwa wa kifikra unavyoingiliana na utumwa mwingine kama vile utumwa wa kimapenzi na utumwa wa kijadi. Ni kutokana na kuingiliana huku tumeweza pia kubaini utumwa ambao ni mbaya kuliko mwingine. Ili kufikia lengo la makala hii, kazi zilizochunguzwa ni *Uhuru wa Watumwa* (1934), *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1987), *Kwaheri Iselamagazi* (1992) na *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1992). Kazi hizi ziliteuliwa kutokana na kuakisi kategoria mbalimbali za utumwa kama inavyofafanuliwa katika makala hii.

**3.0 Utumwa na Fasihi: Mikabala na Matokeo**

Masuala kuhusu utumwa na fasihi yametafitiwa kwa mikabala anuwai. Kwa mfano, wataalamu mbalimbali kama vile: Miers (2000), Welch (2009) na Henry (2020) wametafiti na kubainisha aina mbalimbali za utumwa katika kazi za fasihi. Kwa ujumla, wanabainisha aina kuu mbili za utumwa ambazo ni utumwa wa kijadi na utumwa wa kisasa. Mathalani, Welch (2009) anasema maana ya utumwa iliyokuwapo awali kuhusu utumwa wa kijadi ilibadilishwa kulingana na mabadiliko yanayoendelea kutokea. Anafafanua kuwa, mbali na utumwa wa kijadi, utumwa wa kisasa unabainishwa katika makundi anuwai kama vile: utumwa wa kifikra, ajira ya watoto wadogo, ndoa za kulazimishwa na za utotoni, kukimbilia ughaibuni, utumwa wa kidini, kazi za kulazimishwa na utumwa wa madeni.

Aidha, Lovejoy (2000) anabainisha aina anuwai za utumwa ambazo ni: utumwa wa kumilikiwa kama mali, utumwa wa majumbani, utumwa wa kutumikia madeni, utumwa wa kijeshi, utumwa wa kijinsia, utumwa wa kazi, utumwa wa kuuzwa nje, utumwa wa kiukoo, utumwa wa kivita au kimahakama, na utumwa wa Kiislamu. Anasisitiza kuwa aina hizi za utumwa zinaingiliana kulingana na maeneo na nyakati tofauti, na kwamba utumwa barani Afrika ulikuwa wa kubadilika, ukiongozwa na mahitaji ya ndani pamoja na shinikizo kutoka nje kama biashara na ukoloni.

Sawa na Lovejoy, Stilwell (2014) anajadili tofauti za aina za utumwa zilizojitokeza barani Afrika kwa kuzingatia muktadha wa kijamii na kiutawala. Anaeleza kwamba, kuna utumwa uliojitokeza katika mazingira yasiyo na mamlaka madhubuti ya kiutawala. Aina hii ya utumwa ilijitokeza kupitia mahusiano ya kifamilia, ukoo, uvamizi wa mateka, au uhamasishaji wa mateka kujiunga na jamii mpya. Hii ilifanyika katika jamii zisizo na serikali kuu madhubuti. Stilwell anaendelea kufafanua kuwa kulikuwa pia na utumwa ndani ya mifumo imara ya utawala. Katika jamii zenye mamlaka ya kiutawala iliyopangwa, watumwa walitumika kama nguvukazi ya kisiasa, kijeshi au kiuchumi. Mwisho, kulikuwa na utumwa kwa malengo ya kukuza uchumi ambapo watumwa waliingizwa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo, uchimbaji wa madini, na

biashara. Katika muktadha huu, watumwa walikuwa sehemu muhimu ya uzalishaji mali na ubadilishanaji wa bidhaa. Ingawa Stilwell hakuziorodhesha kategoria hizi kwa mpangilio wa moja kwa moja, alisisitiza kuwa tofauti ya aina za utumwa iliathiriwa na masuala mbalimbali kama vile miundo ya kijamii, majukumu ya kiuchumi ya watumwa na mwelekeo wa maisha ya mtumwa. Kwa ujumla, Stilwell anaonesha kuwa utumwa barani Afrika haukuwa wa aina moja bali ulibadilika kulingana na mazingira ya kijamii, kiutawala, na kiuchumi. Aina hizi za utumwa ndizo zinazorejelewa kama kategoria za utumwa katika makala hii.

## 4.0 Kategoria za Utumwa katika Kazi Teule za Fasihi ya Kiswahili

Katika fasihi ya Kiswahili kuna kategoria mbalimbali za utumwa zinazojitokeza. Kategoria hizo ni utumwa wa kijadi, utumwa wa kifikra, utumwa wa kimapenzi, utumwa wa ndoa za kulazimishwa na za utotoni, utumwa wa majumbani na utumwa wa madeni. Katika kategoria hizo, utumwa wa kifikra ndio wenye nguvu zaidi kuliko aina nyingine za utumwa. Kama inavyofahamika kwa wengi, utumwa wa kijadi ndio uliokuwa unashughulikiwa zaidi kuliko aina nyingine za utumwa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba utumwa wa kijadi unagusa zaidi utu wa nje na kuufanya uonekane zaidi kwa macho. Hivyo, ni rahisi wahusika kuamua kushirikiana kwa hali na mali katika kukabiliana nao, tofauti na utumwa wa kifikra ambao kwa kiasi kikubwa unahusu utu wa ndani. Utumwa wa kifikra hutokea kwa namna isiyoweza kudhihirika waziwazi kwani mtumwa wa aina hii huwa yuko huru kutembea mahala anakopenda pasipo kizuizi chochote kinachoonekana (Badru, 2019). Pamoja na uhuru huo, mtu aliye katika utumwa wa aina hii, fikra zake zimebanwa au kukandamizwa na mafundisho au imani fulani. Aidha, utumwa wa kifikra hudhihirika iwapo fikra za mtu huyo zitaongozwa na mtazamo usio sahihi au unaoweza kuleta madhara kwake au kwa watu wengine. Akizungumza kuhusu utumwa wa kifikra, Stelder (2022) anaeleza kuwa utumwa wa kifikra ni utumwa mbaya zaidi unaoathiri Bara la Afrika na mustakabali wa watoto wa Afrika. Stelder anaendelea kufafanua kuwa utumwa huu unaleta matatizo mengi zaidi yanayoonekana katika bara hili. Utumwa wa kifikra unamfanya mtu ashindwe kufanya maamuzi ya aina yoyote, kwa hiyo, anaweza kuelekezwa kwenye maamuzi mabaya ambayo yanaweza hata kumdhuru yeye mwenyewe. Aidha, nafsi ya mhusika huathirika zaidi kisaikolojia na hukosa uhuru ndani ya moyo (Said na Taib, 2019). Hali hii humfanya mhusika ajichukie na kuona hana faida yoyote katika ulimwengu anaoishi. Kwa hiyo, tunaweza kueleza kuwa utumwa wa aina hii humfanya mhusika akubali hata habari ambazo si sahihi kwa kuwa hawezi kuzifanyia upembuzi yakinifu.

Katika kazi teule zilizotumika katika makala hii, imebainika kuwa mbali na aina hizi mbili za utumwa, umejitokeza pia utumwa wa kimapenzi, utumwa wa madeni na utumikishwaji wa watoto. Utumwa wa kimapenzi ni aina ya utumwa wa kisasa ambao unaathiri mwili, fikra, hisia na utamaduni wa mhusika (Badru, 2019). United Nations Office on Drugs and Crime (UNODC) (2015) wanaeleza

zaidi kuwa uhalifu wa kimapenzi ni njia za upataji wa watu kwa ajili ya kufanya ngono kwa njia zisizofaa kama vile kutumia nguvu, ulaghai au udanganyifu. UNODC wanafafanua kuwa uhalifu wa biashara haramu ya ngono hutokea wakati ambapo nguvu, ulaghai au shuruti hutumiwa kumfanya mtu ashiriki ngono bila ridhaa yake. Nguvu zinaweza kutumiwa ili kumlazimisha mhusika kufanya ngono wakati udanganyifu unaweza kuwa ahadi kama vile za kupata kazi au mahitaji mengine. Kulazimishwa kunahusisha vitisho ambavyo vina madhara kwa mhusika, familia au marafiki wa mwathirika. Kwa upande mwingine, utumwa wa madeni unaelezwa kuwa unawakabili watu na nchi nyingi kwa sasa. Utumwa huu unatokana na mtu kushindwa kulipa deni analodaiwa, hivyo, kuwa mtumwa kwa yule aliyemkopesha. Aina hii ya utumwa imefafanuliwa kuwa inatokana na kuweka dhamana vitu, shughuli au watu unaowamiliki ili kuweza kupata huduma (Miers, 2000). Pia, utumwa wa aina hii hutokana na kushindwa kutimiza makubaliano yaliyowekwa kati ya mtu na mtu au kati ya viongozi na wanajamii (Nichols, 1952). Vilevile, kuwatumikisha watoto ni tatizo lingine lililoenea sehemu nyingi katika nchi zinazoendelea (Canagarajah na Nielsen, 1999). Watoto wanaorejelewa katika makala hii ni wale walio chini ya umri wa miaka kumi na minane. Ingawa baadhi ya kazi wanazofanya zinaweza kuchangia katika ukuaji wa mtoto na chanzo cha mapato ya familia zao, mamilioni ya watoto duniani kote wanalazimishwa kufanya kazi za uharibifu au za kinyonyaji sana (Canagarajah na Nielsen, 1999). Katika mazingira ya kitumwa, watoto wananyimwa haki yao ya elimu na maisha yao yanakuwa ya shida kutokana na kukosa ujuzi unaohitajika katika soko la ajira (Bickford na Rich, 2014). Katika sehemu inayofuata makala inajadili namna kategoria hizi za utumwa zilivyojitokeza katika kazi teule za fasihi ya Kiswahili.

### 4.1 Utumwa wa Kifikra

Kama ilivyoelezwa awali, utumwa wa kifikra hauonekani kwa macho ingawa unagusa maeneo mbalimbali ya maisha ya binadamu. Huleta madhara ambayo hayaonekani kwa haraka kutokana na kugusa utu wa ndani wa mhusika. Hali hii hufanya mchakato wa kukabiliana na utumwa huu kuwa mgumu ukilinganishwa na ule wa kijadi. Kimsingi, utumwa wa kifikra ni matokeo ya imani potofu, mila potofu, elimu isiyochochea udadisi na dhaifu pamoja na matumizi mabaya ya mafundisho ya dini kwa wanajamii (Razi, 2016). Utumwa wa kifikra umejitokeza kwa kiasi kikubwa katika kazi teule za fasihi zilizotumika katika makala hii. Mathalani, katika riwaya ya *Kwaheri Iselamagazi*, wanajamii walikuwa na fikra potofu dhidi ya Matumula na Isamba. Waliamini mambo bila kufanya uchunguzi wa kina, kwa mfano, kutokana na uzushi wa baadhi ya watu, jamii nzima iliamini kuwa Isamba alikuwa mchawi. Hakuna aliyefanya uchunguzi wa kina kuona kama shutuma zilizoelekezwa kwa Isamba zilikuwa na uhalisia. Badala yake, jamii iliamini kuwa Isamba ndiye aliyemroga mumewe Matumula kama mazungumzo ya Njelele na rafiki yake Lina yanavyoonesha:

> [Njelele]: "Shoga, nakwambia mwanamke yule ni mchawi, kamloga mumewe."
>
> [Lina]: "Kweli dada, upole wa Matumula siyo wa kawaida, huko ni kulogwa tu."
>
> "Mwanamume amekuwa bwege kupindukia. Kulogwa huko ndugu yangu'' (Mapalala, 1992: 22).

Imani hii ya kishirikina kuhusu Isamba haikuishia kwa hawa marafiki wawili bali ilienea hata kwa wazee wa ukoo wa Matumula kama anavyoeleza mjomba wake, Mzee Komolo pamoja na dada yake Bibi Ndende kwenye kikao cha ukoo mtawalia:

> "Sisi nduguzo na wazee tumekuita … kukupa ushauri wa maisha. … angalia unavyodidimia, umeshindwa kujiendeleza na hadhi yako kwa watu inashuka. Mwanangu hali hii inatokana na wewe *kufungwa kamba.*[4] Upende usipende *mwanangu umefungwa*."
>
> "Watu wote wanataka kukufanya mtemi, lakini umekataa. Yote haya yanaonesha jinsi ulivyo na akili ndogo. Nayo yanatokea kwa sababu ya huyo mkeo aliyekupumbaza kwa madawa. Huyo ni mwanamke mwasherati na mchawi. ... Huyo *mkeo mshenzi ndiyo kamba iliyokufunga*. Sisi nduguzo lazima tukueleza." (Mapalala, 1992: 35-36).

Katika nukuu hapo juu, mbali na Isamba kutuhumiwa kumroga mume wake Matumula, inaelezwa pia kuwa 'amemfunga kamba' ikiwa na maana kuwa Isamba amemfanya Matumula kuwa mtumwa wake, haelewi anatakiwa kufanya nini kama mwanamume. Hali hii inamshushia hadhi na anashindwa kujiendeleza. Aidha, jamii inaamini kuwa Matumula anakataa kuwa kiongozi kwa maelekezo ya mkewe Isamba. Hali hii inatokana na Isamba kumpumbaza mumewe kwa dawa ambazo inaelezwa kuwa ni 'kamba iliyomfunga."

Kwa upande mwingine, katika utumwa wa kifikra, 'watumwa' wanaungana ili kuuendeleza utumwa huu. Mathalani, wahusika Lina na Njelele wanashirikiana na kupanga namna ya kumdidimiza zaidi Isamba. Kwa mfano, wanamtuhumu Isamba kwamba ana mahusiano ya kimapenzi na Fuhafuha (mhusika ambaye Isamba alizoea kuzungumza naye), Njelele anamwambia Lina:

> Mimi nitachukua hatua, Njelele aliazimia. Dada yake si unamjua? Nitamweleza visa hivi toka mwanzo hadi mwisho. Asipoamini nitamwambia aende kupiga ramli kwa Kabasu-Babu ili ukweli ujulikane. Tutaivumilia aibu hii hadi lini? Lina alifurahi, akaunga mkono. Hapo shoga umesema la maana. Hebu shughulikia jambo hili huenda nasi tukafunguliwa mlango wa riziki ama siyo? (Mapalala, 1992: 22).

---

[4] Msisitizo ni wa waandishi wa makala

Nukuu hii inaonesha Njelele na Lina wanapanga kumdidimiza zaidi Isamba. Hata hivyo, Lina ana ajenda binafsi kuhusu Matumula kama inavyoonekana katika maneno yake, 'huenda nasi tukafunguliwa mlango wa riziki'. Lina anataka kuolewa na Matumula ingawa hajapata nafasi, kwa hiyo, lengo la Lina ni kumwangamiza Isamba ili yeye apate nafasi. Hii inaonesha kuwa katika utumwa wa kifikra ni vigumu sana kuweza kufanya jambo lolote kwa ushirikiano kwa kuwa kila mmoja ana nia yake yenye masilahi binafsi ambayo hayajulikani kwa wengine. Hali hii ina hatari sana kwa mtu binafsi na kwa jamii. Ndiyo maana aina hii ya utumwa inaelezwa na Stelder (2022) kuwa ni utumwa mbaya zaidi na unaoangamiza bara la Afrika. Kutokana na hali hii, madhara ya utumwa wa kifikra ni makubwa kwa kuwa yanamwathiri mtu bila kupata msaada wowote. Mathalani, kutokana na Matumula kuelezwa kuwa anarogwa na mkewe, hakuweza kupata msaada wowote ili kujua ukweli wa jambo hilo. Badala yake marafiki zake walimtenga jambo lililomzidishia msongo wa mawazo. Mwandishi anaeleza, 'Hata wale aliowaita marafiki walimpiga chenga. Wote walitaka atengane naye, si majirani tu bali hata ndugu zake. Wote waliamini kwamba Isamba ni mchawi" (Mapalala, 1992: 29). Kutokana na hali hii, Matumula alikuwa hana msaada wowote wa kumsaidia kufanya maamuzi. Alipotafuta msaada kwa Kabasu-Babu, mganga maarufu, naye alimweleza kuwa matatizo aliyonayo yanatokana na mkewe Isamba. Matumula alikasirika sana, hali ambayo ilimfanya abadilike sana kitabia. Mkewe Isamba alipomwuliza, alizidisha hasira yake na kumpiga. Jambo hili lilimkasirisha zaidi Isamba na kuchukua uamuzi wa kujiua kama asemavyo mwandishi, 'Dunia haina wema. Fitina za watu zimemfanya ajiue' (Mapalala, 1992: 53).

Kama ilivyoelezwa na Said na Taib (2019), utumwa wa kifikra kwa kiasi kikubwa humtesa mhusika na kumwathiri zaidi kisaikolojia. Hali hii ndiyo iliyompata mhusika Matumla baada ya kifo cha Isamba. Matumla alisumbuliwa sana na mawazo kuhusu mkewe Isamba. Alijuta kutokana na kudanganywa na watu, ndugu, marafiki na hata mganga kuhusu mkewe Isamba. Alikumbwa na msongo wa mawazo na kukata tamaa kabisa. Hali hii ilimdhoofisha kiafya na hakuna mtu aliyeweza kumsaidia, jambo lililosababisha kifo chake. Kifo cha Isamba na Matumula kinadhihirisha madhara makubwa yanayoweza kusababishwa na utumwa wa kifikra. Hii inathibitisha hoja ya Stedler kuwa ni utumwa unaoleta madhara makubwa kwa jamii. Kwa kuwatumia wahusika Isamba na Matumula, mwandishi ameonesha dhahiri kuwa utumwa huu unahitaji busara ili kubaini ukweli kabla ya kuchukua hatua. Aidha, kwa wahusika wanaotaka kukutawala au kukumiliki kwa namna fulani wanatumia mbinu ambazo hazionekani waziwazi na si rahisi kuzibaini. Katika hali ya kawaida, tunaweza kumlaumu Matumula kuwa alisababisha kifo cha mkewe Isamba. Hata hivyo, ukichunguza kwa makini masimulizi ya riwaya hii yanaonesha kuwa kuna nguvu iliyojificha, ambayo mhusika mmoja si rahisi kuigundua. Aidha, wanaotaka kukumiliki kwa njia za siri wanashirikiana kuhakikisha kuwa wanakupata. Mathalani, familia yote ya Matumula, majirani, marafiki na hata mganga, wote kwa pamoja, walimtuhumu

Isamba kuwa mchawi. Pia, wahusika hawa wana nguvu kubwa na wanamtishia Matumula na kumwekea vikwazo ili amwache Isamba. Ni katika hali hii tunamwona Matumula akifanya jambo ambalo linasababisha kifo cha mkewe na madhara yake yakasababisha kifo chake mwenyewe. Hakika inahitaji mbinu anuwai kuweza kutambua namna utumwa wa kifikra unavyojengwa kwa kuwa madhara yake yanaonekana mwishoni wakati huwezi kufanya jambo lolote lenye tija kama ilivyotokea kwa Matumula.

Akiendeleza hoja kuhusu utumwa wa kifikra, mwandishi wa riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* anatueleza namna mhusika Kijakazi, ambaye kutokana na utumwa wa kifikra, alikuwa tayari kuvumilia mateso ya aina mbalimbali. Kijakazi akiwa mtumwa nyumbani kwa Malik na mkewe, kisha kwa Fuad - mtoto wa Malik, alikuwa tayari kumtumikia bwana wake kwa maisha yake yote. Mwandishi anasema kuwa, "Shabaha kubwa ya Kijakazi katika maisha yake ilikuwa kumfurahisha bwana wake, na kwa hiyo, alikuwa tayari kumfanyia kazi yoyote" (Adam, 1987: 1).

Kutokana na kutaka kumfurahisha bwana wake bila kuangalia haki zake za msingi, Kijakazi anakataa kushiriki katika harakati za ukombozi wa kuondokana na utumwa wa kijadi zilizokuwa zinafanywa na watumwa wenzake. Kijakazi alikuwa tayari ameyatoa maisha yake yote kwa tajiri wake. Juhudi mbalimbali zilizofanywa na rafiki zake Kijakazi ili kumsaidia atoke katika mateso ya utumwa wa kijadi hazikusaidia kwa kuwa Kijakazi hakuwa tayari. Utumwa huu wa kifikra ni mbaya kwa kuwa unahusisha utu wa ndani. Kuwa huru kunahitaji maamuzi ya ndani. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa utumwa uliomkabili Kijakazi ni tofauti na utumwa wa kijadi ambao watumwa wengine waliupitia. Watumwa wengine waliokuwa kwa Bwana Fuad na kwingineko waliweza kuweka mipango ya kuondokana na utumwa huo na wakafanikiwa. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mwingilianomatini, utumwa wa kijadi umeingiliana na utumwa wa kifikra. Utumwa huu wa kifikra ndio unaoonekana kuwa na nguvu kuliko ule wa kijadi kwa sababu watumwa wa kijadi waliweza kushirikiana na kuwa huru. Kijakazi aliyekuwa na utumwa wa kifikra hakutaka kuwa huru kwani aliendelea kushikilia msimamo wake wa kumtumikia tajiri yake. Aidha, hata pale alipopigwa na Bwana Fuad, Kijakazi alifikiri kuwa anastahili kama nukuu ifuatayo inavyoonesha:

> Kwa machovu makubwa aliyokuwa nayo, Kijakazi alikuwa ameegemea nguzo moja ndani ya banda hilo huku ng'ombe wakila majani…. Fuad alimnyemelea Kijakazi kidogokidogo na … akampiga teke la ubavuni. … Ah! Nisamehe Bwana! Alisema Kijakazi huku anahisi maumivu na huku akiona amefanya kosa kubwa asilowahi kufanya. … Nisamehe Bwana! Sintofanya tena. Kijakazi alisema kwa sauti ya hofu (Adam, 1987: 9-101).

Nukuu iliyotolewa hapo juu inadhihirisha kuwa ingawa Kijakazi alikuwa kwenye utumwa wa kijadi, utumwa wa kifikra ulimfanya asione uonevu aliokuwa akifanyiwa na Bwana Fuad. Hata maumivu ya kupigwa hakuyajali bali aliona kuwa

amefanya kosa kubwa ambalo yamkini alistahili kupewa adhabu na Bwana Fuad. Kutokana na hali hiyo anazidi kuomba msamaha kwa bwana wake.

Kutokana na utumwa wa kifikra, Kijakazi hakujishughulisha kwa namna yoyote ile na harakati za kujikomboa kutoka katika utumwa wa kijadi zilizokuwa zinaendeshwa na wafanyakazi wenzake. Msimulizi anaeleza kuwa kazi kubwa ya Kijakazi ilikuwa 'kumfurahisha Bwana Fuad' (Adam, 1987 : 11). Lengo kubwa la Kijakazi ni 'kuonyesha utiifu kwa bwana wake mpaka mwisho wa umri wake' (Adam, 1987: 21). Aidha, kutokana na maisha aliyozea Kijakazi, alipodanganywa na Fuad kuwa yeye ni mmoja wa wanafamilia ili aendelee kumtumikia, alikubali. Ingawa lengo la Fuad lilikuwa kumlaghai, Kijakazi aliamini kuwa anayoelezwa ni kweli na aliendelea kuyafurahia maneno aliyoambiwa na Fuad bila kuyatafakari kwa makini.

Mbaya zaidi, utumwa wa kifikra unamfanya mhusika asijitambue hata pale anapoelezwa waziwazi kuhusu hali anayopitia katika maisha yake ya kila siku. Hali hii iko bayana kwa mhusika Kijakazi. Kutokana na fikra zake kufungwa shambani kwa Bwana Fuad, anapoelezwa na mfanyakazi mwezake Mkongwe [ambaye aliungana na wenzake na kutoroka shambani kwa Fuad] kuhusu maisha yake kuwa hayana thamani yoyote, kwa Bwana Fuad, Kijakazi anamfukuza. Mkongwe anamweleza Kijakazi:

> Wewe mwenyewe hujimiliki. Binadamu unamilikiwa na mwenye shamba kama anavyomiliki kuku na ng'ombe. Hata hao kuku na ng'ombe wana afadhali kuliko wewe kwani wao walau hupata chakula cha kutosha. Wewe hupati chakula cha kutosha (Adam, 1987: 72).

Mkongwe analenga kumfungua macho Kijakazi ili aone umuhimu wa kuondoka shambani kwa Fuad. Hata hivyo, Kijakazi anaona kama Bwana Fuad amedharauliwa kama anavyofafanua msimulizi:

> Siku nzima Kijakazi alifanya kazi huku akiwa na majonzi makubwa. Mkongwe amemtukana Bwana wake, amemwita mwizi, hana adabu, bahili na sifa nyingi nyingine mbaya (Adam, 1987: 72).

Nukuu hizi zinaonesha kuwa ni vigumu sana kwa mhusika aliye katika utumwa wa kifikra kuondokana na hali hiyo kwa kuwa amejenga imani kwa bwana wake na inachukua muda mrefu kumbadilisha fikra hizo. Mwandishi anaeleza kuwa, Mkongwe hakukata tamaa, aliendelea kumwelimisha Kijakazi umuhimu wa kuondoka shambani kwa Bwana Fuad. Baada ya juhudi za muda mrefu, Mkongwe pamoja na Umari [mfanyakazi ambaye alikuwa ameshapata uelewa wa umuhimu wa kuondokana na utumwa wa kijadi] wanafanikiwa kumkomboa Kijakazi kutoka katika utumwa wa kifikra, kama msimulizi anavyosema:

> Kidogo kidogo fikra za Kijakazi zilianza kufanya kazi … Kwa mara ya kwanza Kijakazi alifikiria namna alivyopoteza maisha yake shambani

> pale toka uhai wa Bwana Malik na Bi Maimuna. … [Kijakazi] aliona wakati umefika wa kumpa Fuad ukweli wake’’ (Adam, 1987: 83).

Ni wazi kuwa utumwa wa kifikra, unaua uwezo wa kufikiri. Jambo hili linamfanya mtumwa kukosa ufahamu kuhusu maisha yake. Ndiyo maana mtumwa wa fikra haoni faida ya kubadilisha hali yake ya maisha. Hata hivyo, kama ilivyotokea kwa mhusika Kijakazi, mhusika anapopata ung’amuzi wa nini kinaendelea kwenye maisha yake anapata nguvu na uwezo wa kufikiri na kujitambua na kuona umuhimu wa kuchukua hatua. Mathalani, baada ya fikra za Kijakazi kurudi, anathubutu kumjibu Bwana Fuad, jambo ambalo hakuweza kufanya kabla ya kujitambua, kama nukuu ifuatayo inavyofafanua:

> ‘‘Sikiliza Fuad, mimi nitakufanyia kila utakalo … lakini sitapiga magoti tena kukuvua viatu. Nimechoka, nimechoka roho yangu na utumwa huu usiokuwa na malipo wala hisani’’ (Adam, 1987: 90).

> ‘‘Sikiliza Fuad! Nakuambia wazi, baada ya leo - nakwambia tena - baada ya leo, sitokubali kukutumikia utumwa wa namna yoyote!’’ (Adam, 1987: 94).

Kwa kuchunguza nukuu hizi, ni dhahiri kuwa Kijakazi amebadilika. Si yule aliyekuwa anamnyenyekea Bwana Fuad na kumwomba radhi hata pale alipomfanyia vitendo viovu. Hali hii katika makala hii ni ukombozi wa fikra. Kijakazi sasa amejikomboa kifikra na anatambua anataka nini na nini hataki katika maisha yake. Utambuzi huu unampeleka kwenye ukombozi wa utumwa wa kijadi. Kijakazi anachukua hatua ya kutoka kwenye shamba la Bwana Fuad na kwenda kuungana na wanajamii wengine waliotoka katika mashamba mbalimbali na kupata nafasi ya kuthaminiwa kama wanajamii wengine walio huru. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwa mtumwa wa kijadi kupata ukombozi wa kifikra ili aweze kuchukua hatua stahiki za kuondokana na utumwa wa kijadi.

### 4.2 Utumwa wa Kijadi

Kama ilivyoelezwa hapo awali, utumwa wa aina hii unahusu kutolewa kwa watumwa kutoka katika maeneo yao ya awali na kupelekwa katika maeneo mengine kwa ajili ya kufanya kazi fulani. Katika riwaya teule za makala hii, imebainika kuwa watu walitekwa kutoka katika maeneo yao na kuanza safari kwa ajili ya kwenda kutumikishwa kazi za kitumwa. Kwa mfano, mwandishi katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*, anaeleza kuhusu watumwa waliotekwa kutoka katika maeneo mbalimbali ya bara na Waarabu. Mwandishi anaeleza kuwa Waarabu hawa walikuwa na msafara wa watumwa (wanaume na wanawake) waliokamatwa ambapo kila walipowakamata waliwafunga miguu na mikono kama nukuu ifuatayo inavyoeleza:

> Hao wenyeji waliingiliwa na watu wasiowajua, nao walikuwa wakikamatwa na kufungwa. Maadui hao wengine walikuwa weupe

> wengine weusi. … Wanaume kwa wanawake wote waliopatikana, walishikwa na kukazwa kamba za mikono na za miguu na hao watu wengine waliowashinda nguvu. Watu hao ni wale Waarabu waliokuwa wakitafuta pembe za ndovu na watumwa, wakawauze mbele (Mbotela, 1934: 9-10).

Ni dhahiri kuwa shughuli ya kukamata watumwa ilifanywa na Waarabu (weupe) pamoja na Waafrika (weusi). Baadhi ya Waafrika walikuwa wenyeji waliowasaidia Waarabu katika biashara hiyo ya watumwa. Lengo kubwa la kuwakamata watumwa ni kwenda kuwauza kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali katika nchi nyingine zilizokuwa zinahitaji nguvukazi isiyokuwa na gharama kubwa. Mtumwa wa kijadi alipata mateso ya kisaikolojia na kimwili. Mathalani, msimulizi anaeleza kuwa, ‘watumwa walifungwa na miti mibaya yenye mafundo shingoni mwao, wakiumia sana’ (Mbotela, 1934: 10). Pia, baadhi ya watumwa walipata mateso makali njiani na wengine kupoteza maisha kabla ya kufika walikotakiwa kwenda, kama anavyoeleza msimulizi:

> Walipokuwa wakisafiri hivi, mawimbi yalichafuka sana. Mvua, umeme, ngurumo, na radi zilipiga pande zote. Matanga yalitota maji, na jahazi likaanza kuzama! Ah! Maskini watumwa!... Jahazi lilizama. … Wote walikufa maji (Mbotela, 1934: 31).

Watumwa wa kijadi walikuwa kwenye hatari ya kupoteza maisha hata kabla ya kufika walikokusudiwa kupelekwa kwa ajili ya kufanya kazi fulani. Inawezekana hakukuwa na mipango madhubuti ya kuhakikisha usalama wa watumwa kutoka katika maeneo walikotolewa mpaka walikokuwa wanapelekwa. Ndiyo maana mawimbi yalipotokea baharini hakukuwa na mipango yoyote ya kuwaokoa watumwa, hivyo, watumwa wote waliachwa wafe. Hii inaonesha kuwa katika utumwa wa kijadi watumwa hawana thamani na kila mara si tu wanakuwa kwenye mateso bali pia katika hali hatarishi.

Hali ya utumwa wa kijadi ambapo watu wanatumikishwa inajitokeza pia katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuadi* ambapo wafanyakazi wanatumikishwa katika mashamba ya wakoloni. Wafanyakazi hawa waliotoka maeneo mbalimbali wananyimwa haki zao za kimsingi. Msimulizi akieleza kuhusu hali hii anasema: ‘… hali ya wakulima ilikuwa mbaya. Mateso ya mabwana shamba ambao waliungwa mkono na wakoloni yalizidi. Ilikuwa hakuna lolote la kufanya isipokuwa kutafuta njia ya kuepukana na mateso hayo’ (Adam, 1987: 25).

Kwa upande mwingine, mwandishi wa riwaya ya *Kwaheri Iselamagazi* anaeleza namna Lumbesi na wanakijiji wengine walivyoingizwa utumwani walipokuwa katika kusherehekea ushindi wa kumuua simba mla watu. Mwandishi anabainisha kuwa wanakijiji hao walipokuwa katikati ya sherehe, walivamiwa na kundi kubwa la Waarabu, Waugwana (wafuasi wa Waarabu) na askari na wapagazi wa Kinyamwezi. Baada ya kukamatwa kama ilivyoelezwa katika riwaya nyingine, walikabiliwa na mateso kama anavyoeleza msimulizi: ‘Mateka wote, wanaume kwa

wanawake, walifungwa shingoni kongwa za miti kama wanyama. Baadhi yao walifungwa viunoni kwa minyororo na kamba nene' (Mapalala, 1992: 26).

Akiendelea kufafanua mateso waliyopata watumwa wakiwa njiani kupelekwa kufanya kazi katika mashamba ya Bwana Tiputipu huku wakiwa wamebeba pembe za ndovu, msimulizi anaeleza kuwa Bwana Sefu, mtoto wa Tiputipu, alimwua vibaya mtumwa kwa lengo la kujaribu bunduki aliyopewa zawadi ya kumpelekea baba yake.

Mateso makubwa ambayo watumwa walikuwa wanapata yanaelezwa kwa namna ya kufanana. Riwaya ya *Kwaheri Iselamagazi* ilichapishwa miaka 58 baada ya ile ya *Uhuru wa Watumwa*, hata hivyo, namna ya kueleza mateso ya watumwa inafanana. Hii inadhihirisha kuwa waandishi wa kazi za fasihi wanapata malighafi ya kazi zao kutoka katika matini - simulizi au andishi zilizopo katika jamii (Kristeva, 1969). Aidha, masimulizi yaliyotolewa kwenye nukuu kuhusu mateso na vitisho walivyopata watumwa yanaendana na mawazo yaliyotolewa na Moniz (2014) kuwa watumwa walikuwa wanapata mateso na vitisho ambavyo vilikuwa havivumiliki.

Pia, msimulizi katika riwaya ya *Kwaheri Iselamagazi* anaeleza namna ambavyo watumwa wanakata tamaa ya kubadilisha maisha yao kutokana na kuzoea mateso. Hii inadhihirisha kuwa ingawa watumwa wanakabiliwa na utumwa wa kijadi, pia wana athari za utumwa wa kifikra. Haya yanaelezwa na mhusika Chitele anapozungumza na mhusika Lumbesi:

> Sikiliza Lumbesi, … kizazi chetu ni cha kilio na mahangaiko. Haya ndiyo majaliwa yetu, na jamii nzima haina njia ya kujiokoa na janga lililopo kwa hivi sasa. Tumefungwa si kwa kongwa za shingo peke yake bali pia kwa kongwa nyingine zilizofanikiwa kutumikisha hata akili zetu (Mapalala, 1992: 105-106).

Katika nukuu hii mhusika Chitele anaweka wazi namna utumwa wa kifikra unavyowatesa wanajamii ambao wapo katika utumwa wa jadi. Ni dhahiri kuwa wanajamii wanapokuwa katika utumwa huu, ni vigumu kuweza kufanya mabadiliko. Hii ni kwa sababu kule kujitambua kwamba wanateswa hakutoshi bila kuwa na ujasiri wa kuchukua hatua madhubuti za kutoka katika mateso hayo. Hali hii inatokana na utumwa wa kifikra na kumilikiwa kiakili kiasi cha kuwafanya wahusika kushindwa kuchukua hatua yoyote inayolenga kuleta mabadiliko chanya.

Utumwa wa kijadi unajitokeza pia katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Riwaya hii inabainisha namna ambavyo watumwa walifanyishwa kazi katika shamba la mkonge, ambalo lilikuwa zao kuu la biashara ya mkoloni wa Kiingereza nchini Tanzania (Tanganyika wakati huo). Mathalani, mtumwa hakuruhusiwa kutoka katika shamba la tajiri wa kigeni, Tumbo Tumbo. Mwandishi anafafanua namna ambavyo watumwa hawa waliojulikana kama manamba walivyozuiliwa kambini katika mashamba ya tajiri na hawakuruhusiwa kutembelewa na mtu yeyote. Katika riwaya hii, kama zilivyo riwaya nyingine teule, mwandishi anaweka bayana namna ambavyo watumwa walidharauliwa na

kuonekana kitu kisichofaa. Mathalani, mwandishi anaeleza namna Mzee Jabiri, ambaye ni mtumwa, alivyoumia vibaya akiwa anafanya kazi kwenye shamba la mkonge na kufa kutokana na kuchelewa kupatiwa matibabu. Badala ya kuzikwa kama binadamu wengine, anatupwa sehemu ambayo haistahili kwa binadamu kama nukuu inavyoonesha:

> Haya mashimo makubwa ya kuzika mavi kwa Bwana Tumbo Tumbo ndiyo yalikuwa pia makaburi ya manamba wa shambani kwake waliofariki hapo. Kwenye hayo mavi ndimo usiku huo Mnyampara Munubi na huyo mtoto wa marehemu - Saidi walimofika kutupa maiti ya Mzee Jabiri wamesimamiwa na Bwana Tumbo Tumbo akiwahimiza kwa kuwafokea (Ruhumbika, 1995: 19-20).

Nukuu hapo juu inaonesha kuwa watumwa walikuwa hawana haki ya kuzikwa kwa heshima kama binadamu. Msimulizi anaeleza namna maiti ya Mzee Jabiri ilivyotupwa kwenye shimo lenye mavi kwa sababu ni mtumwa. Hali hii inaonesha kiwango cha juu cha dharau aliyopewa marehemu Mzee Jabiri, ambaye ni mtumwa. Katika hali ya kusikitisha, Bwana mwenye shamba hana huruma hata kwa mtoto wa marehemu Saidi ambaye bado ni mtoto mdogo wa miaka kumi kushuhudia unyama wa maziko ya baba yake.

### 4.3 Utumwa wa Kimapenzi

Kama ilivyojadiliwa katika sehemu ya 3.0, utumwa wa kimapenzi ni aina ya utumwa wa kisasa ambao unaathiri mwili, fikra na hisia. Aidha, aina hii ya utumwa ina athari kubwa za kisaikolojia kwa sababu hazionekani waziwazi (WHO, 2012). Utumwa huu umejitokeza katika kazi teule zilizotumika katika makala hii. Mathalani, katika riwaya ya *Kwaheri Iselamagazi* ambapo, licha ya Isamba kuandamwa na utumwa wa kifikra, alikabiliwa pia na utumwa wa kimapenzi. Ijapokuwa Isamba alikuwa mke wa Matumula lakini alipokea ujumbe mara kwa mara kutoka kwa Tambwe-Manoti, mtemi wa Urua kupitia msaidizi wake Zaizai kwamba aachane na mumewe Matumula na kuolewa na mtemi kama mazungumzo kati ya Zaizai na Isamba yanavyoonesha:

> ‘‘Mwanamama, hapo baadaye Mazoe atakuletea mzigo wa shanga na bangili - zawadi yako kutoka kwa mtemi ambaye haishi kukuwaza na kutafuta njia ya kukutoa hapa.’’ Isamba alisimama macho yake yakiangalia sakafu. Alinyamaza kimya asiseme lolote. ‘‘Hivi husikii nikuambiavyo?’’ Isamba alinyamaza. ‘‘Bahati gani kupendwa na mtemi. Wenzako wanaililia nafasi wasipate. Fikiri vema usije ukajuta, nakueleza.’’ … [Isamba] ‘‘Nakuambia miye nimeolewa, siwezi kumwacha mume wangu’’ (Mapalala, 1992: 20).

Katika nukuu, Zaizai anaweka wazi kuwa mtemi Tabwe-Manoti anataka Isamba amwache mume wake kama alivyoweka wazi, ‘‘haishi kukuwaza na kutafuta njia ya kukutoa hapa.’’ Ingawa, Isamba ni mke wa Matumula, Zaizai anaona kuwa

kitendo cha mtemi kumtaka kwa nguvu ni kizuri na ni bahati ambayo wanawake wengi wanaitamani. Pia, Zaizai anamsisitizia Isamba kuhusu umuhimu wa kukubali ujumbe wa mtemi na hoja kuwa yeye ni mke wa Matumula siyo tatizo kwa kuwa wanaweza kufanya jambo lolote ili asiwe kikwazo kama anavyoeleza Zaizai katika nukuu ifuatayo:

> Hii habari ya mume isikubabaishe. Twaweza kumtuma safari ya mbali ambayo kurudi ni majaliwa … Isitoshe tunazo njia nyingi za kumsaidia kufupisha maisha yake. … ‘‘Miye niko tayari kufa, lakini sintamwacha mume wangu Matumula.’’ (Mapalala, 1992: 21).

Utumwa wa ngono si tu unamwathiri mhusika moja kwa moja, bali unawaathiri pia watu wengine wa karibu. Katika nukuu, Zaizai anaweka wazi kuwa kama kikwazo ni Matumula mume wa Isamba, basi wanaweza ama ‘‘kumtuma safari ya mbali ambayo kurudi ni majaliwa au kufupisha maisha yake.’’ Hata hivyo, baada ya Isamba kusisitiza kuwa hawezi kukubaliana na mapendekezo ya mtemi, inaonekana kuwa anakwenda kinyume na mfumo uliozoeleka katika jamii. Mfumo kubalifu wa jamii ni kuwa, mtemi hawezi kukataliwa na mwanamke yeyote anayemtaka kimapenzi. Kaida hii inamsukuma Zaizai katika hatua nyingine ya kutumia vitisho, anasema:

> ‘‘Usiwe mjinga, mimi ntarudi na jibu gani kwa mtemi?’’ ... ‘‘Wewe mama utakuja nikumbuka. Miye naondoka na hapana ya mtemi, unasikia? Naondoka na hapana ya mtemi’’ (Mapalala, 1992: 21).

Kwa hiyo, Zaizai anaona kuwa jibu alilopewa na Isamba hawezi kulipeleka kwa Mtemi Tambwe-Manoti, ndiyo maana anamtishia na kumwonya Isamba kuhusu uamuzi wake wa kukataa. Vitisho vinavyotolewa na Zaizai kwa Isamba vinaendana na taarifa za tafiti za utumwa wa kimapenzi zinazoweka bayana kuwa, ikiwa mbinu ya ushawishi inashindikana, wahusika wanatumia vitisho (de Lamotte na Brandt, 2013). Isamba, kama nukuu zilivyobainisha, amekuwa tofauti na wanawake wa nchi ya Urua ambao walikabiliwa na utumwa wa kimapenzi. Kutokana na kaida na taratibu za jamii, endapo mtemi wa nchi yao angetaka kuongeza mke, iwe ameolewa au hajaolewa, ilimlazimu mwanamke husika kuolewa na mtemi bila kipingamizi; awe ameridhia au la.

Utumwa wa ngono unaingiliana na utumwa wa kifikra. Wakati Isamba anakataa waziwazi kulazimishwa kumwacha mume wake anayempenda na kuolewa na Mtemi Tambwe-Manoti, wapo wanawake wanaotamani nafasi hiyo. Nukuu ifuatayo inaonesha namna ambavyo mhusika Njelele anashangaa kwa nini Isamba (mke wa Matumula) anakataa kumwacha mume wake na kuolewa na mtemi:

> Yaani unataka kusema kuwa Isamba amekataa kuolewa na mtemi? … Basi huyo mwanamke ana wazimu ... Mimi ninaona ni kawaida kwa mtemi kumtaka mwanamke yeyote hata kama ameolewa. Hivyo Isamba

> ana mambo yake tu. … hana sababu ya kumkataa mtemi (Mapalala, 1992: 23-24).

Kutokana na utumwa wa kifikra alionao Njelele, anaona kuwa Isamba ana shida. Katika muktadha huu, Njelele haoni kama yeye ana shida kwa kutokujua umuhimu wa mtu kuridhia kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mtu fulani. Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 3.1, utumwa wa kifikra ni tatizo ambalo hata mhusika mwenyewe hajui kama yeye ana shida, badala yake anaona watu wengine ndio wenye shida. Hali hii ndiyo iliyotokea kwa mhusika Njelele ambaye anaona kuwa tatizo analo Isamba badala ya wanawake kama yeye ambao hawajui haki zao za msingi katika mahusiano ya kimapenzi.

Naye mhusika Nzoka katika *Miradi Bubu ya Wazalendo*, aliweka wanawake wengi katika utumwa wa kimapenzi. Miongoni mwa wanawake hao ni Rosemary aliyekubali kushawishiwa na Nzoka, Mwenyekiti-Mtendaji wa Shirika la Miradi, Mali, Akiba na Maendeleo. Kutokana na uwezo wa kiuchumi aliokuwa nao Nzoka, ingawa alikuwa na familia yake, aliweza kubadilisha kabisa maisha ya Rosemary. Haya tunayaona kwa Nzoka kama anavyosema alipomrudisha Rosemary nyumbani baada ya kufanya naye ngono ofisini: ‘‘Wewe siyo mwanamke wa kukaa kwenye zoo kama hii’’ (Ruhumbika, 1995: 118). Badala yake Nzoka alimpangishia Rosemary nyumba kubwa ya vyumba sita ambayo ilikuwa na vitu vya thamani ndani. Pia, alikuwa na teksi maalum ambayo ilikuwa inampeleka ofisini, kumrudisha nyumbani na kumpeleka sehemu yoyote aliyotaka kwa gharama za Nzoka. Kutokana na kushawishiwa na nguvu za kiuchumi, mhusika Rosemary anaishi katika utumwa wa kimapenzi.

Vilevile, katika *Kasri ya Mwinyi Fuad*, mara kwa mara Fuad aliwataka watumishi wake wawe na mahusiano naye ya kimapenzi bila ridhaa yao. Kwa mfano, alitaka kumkamata kwa nguvu Mariam akiwa kwenye banda la ng’ombe lakini kutokana na Mariam kutoridhia, alipiga kelele na kukimbia kama nukuu ifuatayo inavyofafanua:

> Siku moja Mariam alikuwa ndani ya banda la ng’ombe anawapa majani. Fuad alimwona alipokuwa anaingia ndani ya banda hilo akamfuata. ‘‘Mariam hebu njoo nikwambie kitu mara moja’’. Fuad alisema taratibu. … ‘‘Unajua Mariam yako maneno kila siku nilitaka kukwambia lakini sijakupatia nafasi.’’ Maneno gani Bwana?’’ ‘‘Maneno gani?’’ ‘‘Sogea hapa basi nikwambie.’’ … Hakuwahi kumaliza kusema aliyotaka kusema mara alimvamia Mariam na kuanza kumbusu mashavuni. ‘‘Sitaki! Sitaki! Unanikamata kwa nguvu!’’ Mariam alipiga kelele (Adam, 1987: 12).

Bwana Fuad anaona kuwa ana haki ya kumkamata kwa nguvu Mariam ambaye alikuwa mtumwa kwenye shamba lake. Bahati nzuri Mariam aliweza kukimbia na kutoka salama katika mikono ya Fuad siku hiyo. Hata hivyo, Fuad aliendelea kumfuatilia hadi Mariam aliamua kutoroka shambani kwa Bwana Fuad. Kwa

ujumla, utumwa wa kimapenzi ni utumwa unaowatesa wanawake wengi na kuwasababishia madhara.

**4.4 Utumwa wa Madeni**

Utumwa wa madeni, kama ulivyojadiliwa katika sehemu ya 3.0, umejitokeza pia katika kazi teule za makala hii ambapo watu waliingia utumwani kwa kupenda au kutopenda kutokana na madeni yaliyokuwa yanawakabili. Hii ni ishara kwamba utumwa huu pia upo katika jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kwaheri Iselamagazi,* Zaizai anawaeleza wanajamii kuhusu mbinu mpya ya kupata watumwa. Mbinu hii ni kutumia wanajamii watakaoshindwa kulipa ushuru katika nchi ya Urua kama msimulizi anavyoeleza: ‘‘Hivi karibuni, tunatarajia kuanza biashara ya watu, kila kijiji chenye wahalifu na ambacho kitalegalega kutoa ushuru kitalazimika kutupatia watu ishirini wenye afya ambao Tambwe-Manoti atawauza kwa Msiri huko Katanga’’ (Mapalala, 1995: 14). Katika nukuu tunaona kuwa utumwa wa madeni unazua utumwa wa kijadi, na huu ni mwingilianomatini wa kategoria za utumwa tunaouzungumzia katika makala hii. Tunaona wazi katika nukuu kuwa, kama kijiji kinafanikiwa kulipa ushuru bila kulegalega, wananchi wake hawatachukuliwa na kuuzwa kama watumwa.

Kihistoria, inafahamika kuwa utumwa wa madeni ndio sababu hasa ya kuanzishwa kwa mfumo wa manamba ambapo sehemu nyingine ilijulikana kama ‘*kipande system*[5]’ (Mishombi, 1992). Wakoloni ndio walioanzisha utaratibu wa kudhibiti mienendo ya wafanyakazi katika maeneo ya mijini na mashambani. Mwafrika alitakiwa kuwa nacho kila alipokwenda (Mishombi, 1992).

Katika mashamba, manamba walijiandikisha na kupewa maeneo ya kufanya kazi ili kupata fedha za kuendesha maisha yao. Mwandishi wa riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo* anabainisha kuwa watu wengi walikuwa manamba katika mashamba makubwa ya mkonge yaliyokuwa yanamilikiwa na wakoloni katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ikiwamo Morogoro, Kilosa, Korogwe, Mombo na Tanga. Katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*, Mzee Jabiri alipenda mwenyewe kuungana na msafara wa wakimbizi kwenda kutumika katika mashamba ya manamba, na hii ni kutokana na hali ngumu ya maisha aliyokuwa anapitia baada ya kufiwa na ukoo wake mzima. Mwandishi anasema:

> Mzee Jabiri akaamua kujiunga na wakimbizi hao wa Kimakonde kuelekea huko kwenye hiyo manamba ya Wazungu, kwa kupaona mbali ya kutosha kutoka Masasi iliyommalizia ndugu zake wote duniani, na mahali penye kazi ya kuweza kumsaidia kupata chochote cha kuanzia maisha mapya kokote atakakoishia (Ruhumbika, 1995: 4).

[5] Hiki kilikuwa kipande cha karatasi kilichokuwa na jina la mfanyakazi, anakotoka na mwajiri wake (Mishombi, 1992: 30).

Nukuu inaonesha Mzee Jabiri alilazimika kujiunga na manamba ili apate fedha za kumsaidia baada ya kuondoka kwao Masasi. Kwa hiyo, ugumu wa maisha ndio uliomlazimisha kuingia katika kazi za kipande. Msimulizi anaeleza kuwa: ‘‘Nia yake [Mzee Jabiri] ilikuwa mara tu atakapopata chochote cha kutosha, atafute mahali atakapoweza kupaita nyumbani tena, akae’’ (Ruhumbika, 1995: 6). Hata hivyo, Mzee Jabiri alifariki kwa ajali ya kuchomwa na kitu chenye ncha kali kwenye jicho akiwa katika shamba la mkonge la Bwana Tumbo Tumbo alikokuwa anafanya kazi na kufariki. Utumwa huu wa madeni unaweza kukomeshwa kwa mtu kulipa deni au kusaidiwa kulipa deni na kuwa huru. Kwa upande wa ‘Kipande System’, baada ya uhuru nchi husika ilikomesha utaratibu huo (Mishombi, 1992).

### 4.5 Kuwatumikisha Watoto kama Watumwa

Suala la ajira kwa watoto katika maeneo mbalimbali duniani kama lilivyojadiliwa katika sehemu ya 3.0 linajitokeza katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Mzee Jabiri alifanya kazi ya manamba na mtoto wake Saidi ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi. Msimulizi anaeleza kuwa awali Mzee Jabiri ndiye aliyeandikiwa ‘kipande’, na baada ya miezi mitatu Saidi naye alianza kuandikiwa kipande baada ya kuonesha juhudi na ustadi wake wa kukata mkonge. Mwandishi anasema:

> Saidi akawashangaza manamba wote hapo shambani, hadi baba yake mzazi, kwa kumudu naye kukata mkonge na kujaza mita ya kutwa. Mnyapara mkuu… ikawa hana budi kumwandikia huyo mtoto mdogo wa miaka kumi naye kibarua chake kamili kila siku (Ruhumbika, 1995: 5).

Saidi, ingawa alikuwa mtoto, aliweza kufanya kazi sawa na mtu mzima. Hata hivyo, kutokana na kuishi kwenye mazingira ya manamba ambako hakukuwa na shule, kulimfanya asipate nafasi ya kuendelea na masomo, ingawa Masasi alikotoka alikuwa anasoma kama msimulizi anavyofafanua: ‘‘Walipotoka huko kwao Masasi alikuwa tayari darasa la tatu kwenye shule ya Misheni ya Msangusangu, pamoja na kuwa yeye ni Mwislamu na alisifiwa na walimu kwa akili darasani’’ (Ruhumbika, 1995:6). Saidi alitoroka katika shamba la Bwana Tumbo Tumbo baada ya kifo cha baba yake Mzee Jabiri akisaidiwa na Munubi. Kutokana na kukosa elimu, alipofika Dar es Salaam, mwenyeji wake, Bibi Ntwara, alimtafutia kazi ya uboi kwa Mhindi. Hapo alifanya kazi mbalimbali kama vile: ‘‘kufua nguo, kusafisha nyumba, kusaidia kupika, kuosha vyombo na kutumwa tangu asubuhi kadi jioni bila kupumzika’’ (Ruhumbika, 1995: 39-40). Ijapokuwa ilikuwa kazi ya kitumwa hasa, bado ilikuwa si kazi ya kumshinda Saidi. Hata hivyo, mtoto wa kiume wa tajiri aliyekuwa na miaka saba alikuwa katili kwa Saidi. Hivyo, kila asubuhi alikojoa na kunya kitandani ili Saidi atakapokuja kufanya usafi, asafishe hiyo mikojo na mavi, kazi ambayo Saidi aliifanya kwa miezi mitatu na nusu hadi ilipojulikana. Baada ya kujulikana, mtoto huyo wa kiume aliacha hiyo tabia. Kutokana na juhudi aliyokuwa nayo Saidi, alipewa kazi za kusaidia dukani kwa Mhindi. Baadaye, aliajiriwa katika

ofisi za TANU wakati wa harakati za kupigania uhuru na baada ya uhuru aliajiriwa Ikulu kama mesenja. Ingawa Saidi alikuwa na juhudi ya kufanya kazi mbalimbali, hakuwa na elimu wala ujuzi wowote ambao ungemsaidia kupata kazi nzuri. Kutokana na kazi aliyofanya, aliishi maisha ya hali ya chini tofauti na wenzake waliokuwa na elimu na ujuzi kama Nzoka. Hali aliyopitia mhusika Saidi inaendana na hoja zinazotolewa na watafiti tangulizi kuwa utumwa kwa watoto unawafanya wakose sifa muhimu zinazowawezesha kuingia kwenye ushindani wa soko la ajira (Bickford na Rich, 2014).

## 5.0 Mbinu za Kuondokana na Utumwa wa Kijadi

Miongoni mwa sifa za utumwa wa kijadi ni kuonekana waziwazi na madhara yake pia kuonekana dhahiri kwa wahusika. Madhara haya yanapozidi, watumwa wanachukua hatua za wazi na kujikomboa. Mathalani, katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, baada wafanyakazi kuchoshwa na manyanyaso ya Bwana Fuad, wanaungana na kufanya mapinduzi. Kufanikiwa kufanya mapinduzi kunatokana na umoja, ushrikiano na ujasiri wa hali ya juu. Kwa mfano, mwandishi anasema kutokana na dhiki walizokuwa nazo watumwa katika mashamba mbalimbali, hawakwisha kufanya migomo na mikutano ya kudai uhuru kutoka kwa wakoloni. Hata hivyo, haikuwa rahisi kwa kuwa kila wakati walikabiliwa na vizuizi mbalimbali kama nukuu inavyoeleza:

> Kila wafanyakazi walipochukua hatua za kudai haki zao, waliitiwa maaskari wa kikoloni ambao walitumia silaha zao za virungu, mabomu ya kuumiza macho na bunduki kuwatawanya. Baadhi ya viongozi wao na wafanyakazi wengine jasiri walitiwa vifungoni ambako waliteswa na kufanyiwa ukatili wa kila aina (Adam, 1987: 11).

Nukuu inaonesha kuwa haikuwa kazi rahisi kupata haki kwa wafanyakazi waliokuwa katika mashamba mbalimbali ya wakoloni. Hata hivyo, wafanyakazi walishirikiana na mwishowe wakafanikiwa kuipindua serikali ya kikoloni. Baada ya mapinduzi, wananchi wanakuwa huru na kupata ardhi inayowawezesha kuendesha maisha yao kwa uhuru.

Halikadhalika, katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo* mwandishi anaeleza kuwa manamba walitumikishwa sana lakini walipoona hali inazidi kuwa ngumu waligoma. Migomo ya manamba kwenye mashamba ya mkonge ilikuwa ikitokea mara kwa mara. Hii ni kwa sababu matajiri wa kigeni walikuwa na tamaa ya faida na hawakumthamini mtu mweusi wala hawakumwona kama wao. Waliwatumikisha hadi manamba wakafikia kikomo cha uvumilivu, hivyo wakagoma. Mara nyingi migomo hiyo ilikuwa ikivunjwa na matajiri wa mashamba ya mkonge na manamba waliogoma kupewa adhabu mbalimbali ikiwamo kuchapwa viboko na kupunguziwa mishahara yao. Hata hivyo, watumwa walifanikiwa kupinga mateso kutoka kwa wakoloni kwa kushirikiana hata wakaweza kujikomboa.

Mbinu nyingine iliyotumiwa na watumwa ili kujikomboa ni kutoroka. Kwa ujumla, kutokana na mateso mbalimbali waliyopitia watumwa, hawakuwa tayari kuendelea na maisha ya utumwa. Baadhi ya watumwa walitoroka ijapokuwa hawakufanikiwa, wengine walifanikiwa na kuna walioungana na kufanya mapinduzi dhidi ya watesi wao. Mathalani, katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*, Mtipia alipanga kutoroka na aliwasaidia wenzake kutoroka ijapokuwa hawakufanikiwa kufika mbali kwani walikamatwa. Mwinyi Upate na Pwanali waliwafuatilia watumwa kwenye njia ileile waliyoijia na walipofika magenge ya fisi, walimkuta Mtipia akiwafungua watumwa. Mwinyi Upate alimwambia Mtipia, ‘‘umeniasi, tena wawafanya wengine nao waniasi, mbona basi umeonekana?’’ (uk. 29). Pengine watumwa hawa wangebadili njia na kutumia njia tofauti na ile waliyojia wasingekamatwa.

Kutoroka kwa watumwa na kukamatwa kunajitokeza pia katika riwaya ya *Kwaheri Iselamagazi* ambapo Lumbesi na Ilumba walitoroka lakini walikamatwa baada ya kuonekana wakiwa wanaoga mtoni. Kinachoonekana kwa Lumbesi na Ilumba ni kwamba utumwa wa kimapenzi ulikuwa na nguvu kuzidi ule wa kijadi kwa kuwa walijisahau kwamba walikuwa watumwa na kwamba bado walikuwa katika kutoroka kama nukuu ifuatayo inavyoonesha:

> Baada ya kutembea kwa muda mrefu, waliwasili kwenye kijito cha maji baridi. … Walioga kwa furaha huku wanarushiana maji usoni. … Aliponyanyua macho yake Ilumba aliwaona Waungwana watatu waliovalia majambia na kushika bunduki. … Bwana Hemedi alimfahamu Lumbesi aliyekuwa akigalagala kwa maumivu huku damu ikivuja. ‘‘Ha! Lumbesi! Tumekuona ukioga mtoni. Bila shaka uko mbioni kutoroka mshenzi wee’’ (Mapalala, 1992: 106-107).

Katika nukuu hii huenda kama Lumbesi na Ilumba wasingeingia mtoni na kuanza kuoga na kurushiana maji wangefanikiwa kutoroka na kuanza maisha ya familia ambayo waliyatamani. Kwa hiyo, tahadhari kwa watumwa ni jambo muhimu katika kila hatua ili kuweza kufanikiwa.

Aidha, katika riwaya ya *Kwaheri Iselamagazi*, baada ya Matumula kuokotwa na wapagazi akiwa amezirai kutokana na kunusurika kuliwa katika nchi ya wala watu, aliingizwa katika msafara huo wa wapagazi. Mwandishi anasema, mmiliki wa msafara huo wa wapagazi, Tambwe Manoti, alitaka kumfanya Matumula kuwa mtumwa wake milele. Hata hivyo, kutokana na Matumula kutotaka kuendelea kutumikishwa kama mtumwa, alifanikiwa kutoroka kwa kupiga mbizi baharini hadi alipotokea kwenye nchi ya Ulele ya malkia Umbasi, mama yake Isamba.

Hali ya baadhi ya watumwa kufanikiwa kutoroka inajitokeza pia katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazaledo* ambapo Mnyampara Munubi na mtoto Saidi wanafanikiwa kutoroka katika shamba la Tumbo Tumbo. Munubi ndiye aliyetoa

wazo la kutoroka kwa mtoto Saidi baada ya kutupa maiti ya Mzee Jabari kwenye shimo la mavi kama nukuu ifuatayo inavyoeleza:

> Umeshuhudia wewe mwenyewe jinsi huyu Mzungu alivyomuua baba yako … Halafu sasa ona hii kufuru tunayotoka kufanya kwa amri yake! Funga mizigo yako tuondoke hapa (Ruhumbika, 1995: 24).

> Kulipokucha asubuhi yake Bwana Tumbo Tumbo akaamka hesabu ya manamba shambani kwake imepungua. … Mnyampara Mkuu wake, Munubi, na huyo mtoto wa marehemu, Saidi, nao walikuwa wametambua kwamba hapo shambani kwa huyo tajiri wa Kizungu palikuwa siyo mahali pa binadamu kuishi (Ruhumbika, 1995: 20).

Wahusika Munubi na Saidi wanafanikiwa kutoroka shambani kwa mkoloni na kwenda kuishi maisha huru. Hii inatoa picha kuwa katika maisha ya kitumwa, wapo wanaofanikiwa kutoroka na wengine hawafanikiwi. Jambo muhimu ni kufanya maamuzi ya haraka. Munubi na Saidi, baada ya kuona uovu aliofanyiwa Mzee Jabiri hata baada ya kufa, walichukua maamuzi ya haraka. Pia, walichukua tahadhari wakati wa kuondoka shambani kuhakikisha wanafanikiwa. Kwa upande mwingine, imebainika kuwa Mnyampara Munubi alikuwa na uzoefu na maisha ya utumwa na kutoroka. Msimulizi anaeleza kuwa Munubi alifika katika shamba la Tumbo Tumbo baada ya kutoroka katika shamba la Mreno. Katika shamba la Mreno, alitoroka baada ya kumpiga mkoloni kama nukuu inavyoeleza:

> Bahati mbaya huyo kijana wa Kireno, alipoona anaweza kutukana anavyotaka hilo jitu kubwa kama tembo na bado lisithubutu kusema hata neno moja, akafikiri anaweza kufanya nalo apendavyo na akaingilia kumpiga makofi na mateke. Mnyampara Munubi safari hii akajibu kwa kumpiga huyo karani wa Kireno ngumi moja tu katikati ya kifua, na huyo kijana mwenzake akaanguka chini kama gunia la mchanga na kuzimia na kupelekwa hospitali kwa machele (Ruhumbika, 1995: 23).

Mnyampara Munubi hakuwa tayari kuendelea kunyanyaswa na kijana mwenzake kwa sababu tu alikuwa mkoloni. Hivyo, alichukua hatua ya kujibu mapigo baada ya kijana huyo kuanza kumpiga makofi na mateke. Kijana wa Kireno aliyepelekwa hospitali alifariki. Kitendo cha kumwadhibu mkoloni na kumsababishia kifo kilimfanya Mnyampara Munubi kutoroka katika shamba la Mreno huko Msumbiji na kwenda Tanga kwenye shamba la Tumbo Tumbo ambako nako alitoroka.

Mbali na watumwa wenye kupinga utumwa wa kijadi, watu wengine ambao hawakuwa watumwa kama vile wanaharakati wa ukombozi na wapigania uhuru, walishirikiana kuhakikisha kuwa watumwa wanakuwa huru. Mathalani, katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* mwandishi anatueleza kuwa Waingereza waliwaokoa watumwa waliokuwa wanasafirishwa na Waarabu kwenda katika nchi mbalimbali na kuwasaidia kuwapa makazi huru. Kwa upande wa riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*, mwandishi anaeleza kuwa mwaka 1954, Julius K. Nyerere na wananchi wenzake kumi na sita kutoka sehemu mbalimbali za Tanganyika

walianzisha chama cha TANU chenye siasa ya ukombozi wa Mwafrika. Harakati hizi za ukombozi ndizo zilizoendelea hadi kuiletea Tanganyika uhuru, na kutokana na uhuru huu, watumwa na manamba waliokuwa wanatumikishwa maeneo mbalimbali wakawa huru.

Kwa ujumla, utumwa wa kijadi ulikuwa haukubaliki kutokana na shida na mateso waliyopitia watumwa. Aidha, wengi walipoteza maisha kutokana na kupambana na watesi wao au kutafuta uhuru wao. Uhuru haukupatikana kirahisi bali ulitokana na mikakati mbalimbali waliyokuwa nayo watumwa wenyewe na wanaharakati waliokuwa tayari kupambana na kila mtu au kikundi kilichokuwa kinamiliki watumwa. Kutokana na mikakati hiyo, kuna watumwa waliofanikiwa kutoroka na wengine walifanya mapinduzi. Kwa kiasi kikubwa, haya yote yalifanikiwa kutokana na ujasiri, umoja, mshikamano na ushirikiano uliokuwapo baina ya wahusika na watu wengine walioona hali waliyokuwa wanapitia watumwa.

**6.0 Mjadala Mfupi kuhusu Matokeo ya Utafiti**

Katika aina za utumwa zilizojadiliwa katika makala hii, aina za utumwa ambazo zimejitokeza zaidi katika kazi teule za fasihi ya Kiswahili zilizochunguzwa ni utumwa wa kifikra na utumwa wa kijadi. Utumwa wa kifikra unamsakama mtu ndani kwa ndani na watu wanashirikiana katika kuuendeleza. Kwa mfano, katika *Kwaheri Iselamagazi*, Njelele na wanawake wengine wanashirikiana na wanajamii wengine katika kuendeleza fikra potofu kuhusu Isamba. Wanamtuhumu Isamba kuhusu uchawi, kukosa uaminifu katika ndoa yake na kuwa hana sifa ya mke bora kwa kuwa na mtoto mmoja tu. Aidha, ukweli kuhusu tuhuma zinazoelekezwa kwa Isamba hazijulikani mapema. Mathalani, mumewe Matumula hakujua hila ambazo zilifanywa na watu mbalimbali kama vile – ndugu zake Matumula, majirani, marafiki, viongozi na mganga. Kifo cha Isamba ndicho kilimpa picha halisi Matumula. Aidha, kitendo cha Bibi Ndende kumwomba Lumbesi msamaha kinaonesha kuwa yeye pia alijua ukweli kuhusu Isamba, mke wa kaka yake, kama nukuu inavyoonesha: ‘‘[Bibi Ndende] ‘‘Mwanangu … Mtoto wa Matumula unisamehe baba yangu. … Dunia ilinihadaa.’’ Bibi Ndende alilia kwelikweli. … ‘‘Mwanangu nakuomba unisamehe’’ (Mapalala, 1992: 83). Pia, katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, mhusika Kijakazi aliteswa sana na utumwa wa kifikra. Wakati watumwa wengine wanaendelea na harakati za kujikomboa, yeye aliona kuwa wanamkera bosi wake Bwana Fuad. Aidha, Kijakazi alikuwa tayari kufanya kila jambo linalomfurahisha bwana wake bila kujali kama anaumia au la. Baada ya kushauriwa kwa muda mrefu kuhusu umuhimu wa kuwa huru, Kijakazi anajitambua na kuweza kutoka katika shamba la Bwana Fuad.

Tofauti na utumwa wa kifikra, utumwa wa kijadi unaonekana waziwazi na athari zake zinaonekana mapema. Pia, aina hii ya utumwa imekuwa na matumizi ya mbinu mbalimbali katika jitihada za kujikomboa kama vile watumwa kushirikiana katika kutafuta uhuru wao, watumwa kupigana na wamiliki wao kama alivyofanya Munubi, watumwa kutoroka kama alivyofanya Matumula, Munubi na Saidi,

watumwa kupata msaada kutoka kwa wanaharakati wapigania uhuru au kutokana na harakati za kupinga utumwa, au watumwa kufanya mapinduzi.

Kwa upande mwingine, utumwa wa kimapenzi, unaelezwa kuwa una athari mbalimbali kwa waathirika pamoja na wale walio karibu nao. Mathalani, Isamba anapokataa ujumbe wa kuwa na mahusiano ya kimapenzi na Mtemi Tambwe-Manoti, anahatarisha maisha yake na mume wake. Hata hivyo, kuna baadhi ya wanajamii ambao wapo kwenye utumwa wa kifikra ambao wanaona kuwa Isamba anapoteza bahati aliyopata ya kupendwa na Mtemi Tambwe-Manoti. Kwa upande mwingine, Lumbesi alikuwa na mwonekano mzuri uliomfanya apendwe na wake za mabwana wake. Mathalani, alipofika katika kambi ya Tiputipu, mke wa Tiputipu, Binti Rashidi, alimpenda. Baada ya kupigwa sana kwa kutoroka na Ilumba, mke wa Tiputipu ndiye anayemwokoa Lumbesi na kumuuguza majeraha. Kwa hiyo, kitendo cha Lumbesi kupendwa na mke wa mtemi kinafanya utumwa wa kijadi unaomkabili kuwa na ahueni.

Utumwa wa madeni umebainika kuwa unaingiliana pia na utumwa wa kijadi. Katika kazi teule zilizotumika katika makala hii, wapo viongozi waliokuwa wanawatoa wanajamii kuingia katika utumwa wa kijadi kutokana na kushindwa kutimiza malengo yaliyowekwa na viongozi. Mathalani, katika riwaya ya *Kwaheri Iselamagazi*, baadhi ya watumwa walipatikana kwa njia hiyo. Vilevile, kutokana na ugumu wa maisha, wapo watu waliokuwa tayari kufanya kazi kama manamba kwa utaratibu wa 'kipande' ili kuweza kulipa gharama za maisha.

Makala pia, imejadili namna watoto wanavyotumikishwa. Katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*, tumejadili watoto wanavyopata athari hasi na za kudumu katika maisha yao kutokana na kutumikishwa. Kwa mfano, mtoto Saidi alikuwa anafanya kazi kwa bidii, lakini kutokana na kukosa elimu na ujuzi, ameishi maisha ya shida na familia yake. Pia, anadharauliwa na bosi wake Nzoka ambaye alikuwa na kazi nzuri kutokana na elimu na ujuzi aliokuwa nao. Hii inadhihirisha kuwa watoto wanaoingia utumwani wana hatari ya kukabiliwa na changamoto katika maisha yao yote.

## 7.0 Hitimisho

Kwa ujumla, makala hii imejadili kategoria tano za utumwa kama zilivyojitokeza katika kazi teule za fasihi ya Kiswahili. Katika aina za utumwa zilizojadiliwa, imebainika kuwa utumwa wa kifikra ni utumwa ambao umekuwapo tangu jamii zilipoanza kuwapo. Aidha, matokeo ya utumwa wa kifikra yanaonekana wakati mhusika hawezi kupata msaada kutokana na aina hii kuhusisha zaidi utu wa ndani wa mhusika. Kwa upande wa utumwa wa kijadi, wahusika hushirikiana kwa pamoja na kupanga mbinu anuwai za kujikomboa tofauti na ule wa kifikra. Utumwa wa kimapenzi, mbali na athari hasi, imebainika kuwa mtumwa anaweza kupata athari chanya kulingana na mazingira ya utokeaji wa huo utumwa wa kimapenzi. Aidha, utumwa wa madeni unaweza kuwa chanzo cha utumwa wa kijadi kwa baadhi ya wahusika pale ambapo taratibu za kijamii zinakiukwa. Vilevile, utumwa wa watoto

unawapa watoto athari hasi na za kudumu katika maisha yao yote. Katika mjadala imebainika kuwa aina hizi za utumwa zinaingiliana kwa namna tofauti.

**Marejeleo**

Adam, S.A. (1987). *Kasri ya Mwinyi Fuad.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Alfaro, M.J.M. (1996). Intertextuality: Origins and Development of the Concept. *Atlantis.* 18(1/2): 268-285.

Badru, Z.A. (2019). "Mfumo Dume Chanzo cha Ufungwa wa Mwanamume: Uhakiki wa Semi kutoka Jamii za Kiafrika". *JULACE.* 4(1): 60-69.

Bakhtin, M.M. (2010). *Speech Genres and Other Late Essays.* Texas: University of Press.

Baks, J., Breman A. na Nooij, A. (1966). "Slavery as a System of Production in Tribal Society". Bijdragen tot de Taal-, Land-en Volkenkunde, 122(1), 90-109. http://doi.org/10.1163/22134379-90002942

Bickford, J.H. na Rich, C.W. (2014). *Examining the Representation of Slavery within Children's Literature.* http://thekeep.eiu.edu/eemedu_fac/27

Canagarajah, S. na Nielsen, H.S.(1999). *Child Labor and Schooling in Africa: A Comparative Study.* https://documents1.worldbank.org/curated/en/115421468741868002/pdf/multi-page.pdf

de Lamotte, M. na Brandt, D. (2013). *Sex-Slavery in the Contemporary World*. https://www.sciencedirect.com/science/article/pii/S1474667016342197

Douglass, F. (1845). *Narrative of the Life of Frederick Douglass; An American Slave*. Boston: Anti-Slavery Office.

Equiano, O. (1789). *The Interesting Narrative of the Life of Olaudah Equiano or Gustavus Vassa: The African*. London: Hogarth Blake Ltd.

Henry, G. (2020). Uchambuzi Linganishi wa Ujumi wa Kifasihi katika Simulizi Teule za Watumwa kutoka Afrika, Amerika na Ulaya. Tazmili ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kristeva, J. (1969). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art.* New York: Columbia University Press.

Lovejoy, P. (2000). *Transformations of Slavery in Africa.* Cambridge: Cambridge University Press.

Madumulla, J.S. (2000). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Mapalala, B. (1992). *Kwaheri Iselamagazi*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mbotela, J. (1934). *Uhuru wa Watumwa*. London: Sheldom Press.

Miers, S. (2000). Contemporary Forms of Slavery. *Canadian Journal of African Studies*. 34(3): 714-747.

Mishombi, G.T. (1992). Colonialism and Underdevelopment in Tanzania. *Tanzania Zamani: A Journal of Historical Reseach*. https://journals.co.za/doi/pdf/10.10520/AJA08566518_28.

Moniz, A. (2014). Black Women in American Literature: Slavery through Slave Narratives in Contemporary Fiction. *HOHONU* 3: 32-37.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Nichols, C.H. (1952) Slave Narrative. *Negro History Bulletin*. 15(6): 107-114.

Northup, S. (1853). *Twelve Years A Slave, Narrative of Solomon Northup*. London: Sampson, Low &Company.

Prince, M. (1831). *The History of Mary Prince: A West Indian Slave*. London: F. Westley and A.H. Davis.

Quirk, J. (2012). 'Defining Slavery in All its Forms: Historical Inquiry as Contemporary Instruction'. https://www.researchgate.net/publication/290836326.

Razi, A. (2016). Narratives of Amelioration: Mental Slavery and the New World Slave Society in the Eighteenth-Century Didactic Imagination. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Toronto.

Ruhumbika, G. (1992). *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Said, Z. na Taib, A.H. (2019). *Fasihi ya Ufungwa: Nadharia na Mikabala ya Uhakiki –Riwaya kama Kifani*. Dar es Salaam: Heko Publishers.

Stelder, M. (2022). The Colonial Difference in Hugo Grotius: Rational Man, Slavery and Indigenous Dispossession. *Postcolonial Studies*, *25*(4): 564–583. https://doi.org/10.1080/13688790.2021.1979297 https://documents1.worldbank.org/curated/en/115421468741868002/pdf/multi-page.pdf

Stilwell, S.A. (2014). *Slavery and Slaving in African History*. Cambridge: Cambridge University Press.

United Nations Office on Drugs and Crime (2015). *World Drug Report 2015* https://www.unodc.org/documents/wdr2015/World_Drug_Report_2015.pdf

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Welch, C.E. (2009). "Defining Contemporary Forms of Slavery: Updating a Venerable NGO". *Human Rights Quarterly*. (31)1: 70-128.

WHO (2012). *Understanding and Addressing Violence Against Women: Human Trafficking* http://www.who.int/about/licensing/copyright_form/en/index.html

Worton, M. na Still, J. (1990) *Intertextuality: Theories and Practice.* New York: Manchester University Press.